


# Anansi Na Tai

Brigid Simiyu

Wiehan de Jager

Kiswahili

African Storybook.org



Buibui Anansi na Sungura walikuwa marafiki. Waliishi kwa amani katika kijiji kilichokuwa milimani. Sungura alimiliki shamba kubwa lenye wingi wa mboga na matunda. Ingawa Sungura alikuwa mkarimu na kumgawia rafikiye Anansi, Anansi hakufurahia na alimwonea wivu.



Kwa hivyo Anansi aliwaza juu ya njia barabara ya kunyakua shamba la Sungura. Muda mfupi baadaye, Sungura aliachwa katika hali ya umaskini na bila makao. Anansi sasa alijivunia kuwa mmiliki wa shamba lote la Sungura pamoja na mboga na matunda.



Anansi alienda sokoni kuuza matunda na mboga. Alipata fedha nyingi hata zikajaza kikapu! Alizitumia baadhi ya pesa hizo kununulia nafaka ili kuipelekea familia yake. Aliweka nafaka hiyo juu ya fedha zilizokuwa katika kikapu.



Buibui, Anansi, alielekea nyumbani akiwa amebeba kikapu chake kichwani huku akiimba. Wakati wote huo, alikuwa akiwaza vitu vyote angenunua kwa kutumia fedha zote alizokuwa nazo.



Akiwa njiani, kulikuwa na mvua ya manyunyu. Punde tu manyunyu yaligeuka na kuwa mvua kubwa iliyomwagika. Anansi, Buibui, alikiacha kikapu chake pembeni mwa barabara naye akaenda chini ya mti kujikinga. Lakini alikichunga kikapu chake cha dhamana kutoka pale alikokuwa.



Mvua ilianza kunyesha kwa wingi zaidi na Anansi alihisi baridi na kunyeshewa. Kwa hivyo alikimbilia kwenye shimo. "Nitakaa ndani ya shimo hili hadi mvua itakapokoma kunyesha," Buibui alijiambia. "Bora fedha zangu zimekingwa na nafaka niliyoweka juu yake."



Muda mfupi baadaye, Tai akawa anaruka pahali pale na kuweza kuona kikapu kando ya barabara. Aliona kwamba kulikuwa na fedha na nafaka kaitika kile kikapu. Kwa hivyo alikifunika kikapu na mbawa zake na kusubiri mvua itakapoisha.



Anansi aliona Tai akiwa amekalia kikapu chake. "Ah asante rafiki yangu kwa kukilinda kikapu changu," alimwambia Tai. "Samahani, Anansi, nilikusikia vyema?" Tai alisema. "Kikapu chako? Kikapu hiki ni changu! Nilikipata hapo pembeni mwa barabara!" Anansi hakuweza kuamini masikio yake! "Ni changu, nakwambia!'."



Akiwa amekasirika, Anansi alienda kushtaki wizi huo kwa Chifu. Lakini Tai alimwambia Chifu na wazee wake, "Inawezekanaje mtu kukiacha kikapu barabarani kilichojaa fedha na nafaka bila ulinzi wowote?" "Lakini nilikuwa nikikichunga kikapu changu," alisema Anansi. "Fedha ni zangu na nafaka ni yangu!" "Nilikuwa nimekikinga kikapu kwa mbawa zangu wakati wewe ulitokezea tu na kusema kwamba kilikuwa chako!" Tai alijibu.

Baada ya Chifu na wazee wake kusikiliza kwa makini pande zote mbili, waliwataka Anansi na Tai watoke hapo na kwenda mbali kidogo. Walijadili kisa hicho kwa muda mrefu. Hatimaye, walifikia uamuzi.



Waliwaita tena Anansi na Tai. "Tunaamini usemi wa Tai," walisema. "Yeye si mwizi. Ulikuwa ukijitakia kitu kisichokuwa chako." Anansi, Buibui hakuweza kuamini masikio yake. Aliangua kilio.



Punde tu baadaye, ujembe ulisambaa kwamba uamuzi ulimwendea vibaya Anansi. Alipoondoka, alimsikia Sungura akicheka na kucheka. Sungura alirudi katika shamba lake na kuendelea kupanda matunda na mboga. Lakini Anansi alirejelea hali yake ya umaskini, akiwa bila marafiki.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Anansi Na Tai

**Author** - Ghanaian folktale
**Translation** - Brigid Simiyu
**Illustration** - Wiehan de Jager
**Language** - Kiswahili
**Level** - Longer paragraphs

© African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 4.0
**Source** www.africanstorybook.org